

Mfumo wa Umilikaji, Udhhibiti na Matumuzi ya Rasilimali Asili Nchini Tanzania¹

(Muhtasari wa Matokeo ya Uchambuzi wa Mtafiti na Mapendekezo)

(Kuchochea mjadala tu)

na

Issa Shivji
Profesa wa Sheria
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
ishivji@ud.co.tz

Lengo la Utafiti

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza mfumo wa umilikaji, udhibiti na matumizi ya rasilimali asili katika maeneo kavu ya Tanzania, hususun, mikoa ya kati na kaskazini yakiwemo Dodoma, Arusha na Singida. Maeneo haya hutegemea zaidi ufugaji, uwindaji, utalii na mazao yatokanayo na misitu.

Inakadiriwa kwamba takriban watu 6.5 milioni au asilimia 20% ya Watanzania wote, na karibu nusu ya mifugo nchini, huishi katika maeneo haya. Pia inajulikana, angalau takwimu hutofautiana, kwamba umaskini umekithiri sana vijijini pamoja na viwango vya huduma za lazimu - maji safi, elimu afya, makazi - kushuka ama kupotea moja kwa moja.

¹ Utafiti huu ni mradi wa Chuo Kikuu cha Cambridge kikishirikiana na watafiti kutoka India, Zimbabwe na Tanzania. Utafiti wenyewe unadhaminiwa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza (DfID). Mtafiti anayehusika kutoka Tanzania ni Profesa Issa Shivji wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yaliyomo ni mawazo ya Mtafiti mwenyewe na hayana uhusiano wowote na mawazo au msimamo wa DfID.

Rasilimali asili ambayo ni muhimu kwa wakazi wa maeneo haya ni ardhi yenyewe, malisho, mbuga, wanyama pori na misitu.

Mfumo wa Umilikaji na Utawala

Kwa muhtasari, yafuatayo ni sifa kuu za mfumo wa umilikaji na utawala nchini ambao huathiri moja kwa moja udhibiti na matumuzi ya rasilimali asili nchini.

- 1) Tangu wakati wa ukoloni, ardhi yote ya Tanzania imewekwa chini ya miliki ya Dola/Serikali. Wenyeji hutumia ardhi kwa mujibu wa mila na desturi za jamii yao. Ingawa kisheria matumizi yao ya kimila hutambuliwa, miliki ya kimila haipewi uzito sawa na miliki ya hati. Msimamo huo wa kisera na kisheria umeanza kubadilika katika muungo wa hivi karibuni lakini mwelekeo wenyewe hauna uhakika.
- 2) Miliki ya malisho ya wafugaji kihistoria huwa hauthaminiki. Jamii za wafugaji ni za kwanza kupoteza ardhi na rasilimali asili yao kwa matakwa na maslahi mengine, hususan, wakulima, serikali, makampuni ya uwindaji, miradi ya hifadhi na utalii, na miradi mingine ambayo huitwa miradi ya umma, n. k.
- 3) Kwa kuwa dola ndiyo inayohodhi umilikaji, udhibiti na upangaji wa matumuzi ya rasilimali asili pia ni mikononi mwa vyombo na maafisa wa serikali. Hata hivyo, katika miaka ya sabini, kutokana na kuanzishwa kwa operesheni vijiji, serikali iliweka mfumo wa utawala vijijini, hususan, serikali za kijiji. Vyombo muhimu katika utawala kijijini ni Mkutano Mkuu wa Kijiji (MMK) na Halmashauri ya Kijiji (HK).

- 4) Kinadharia, utawala kijijini hakuna budi kuwashirikisha wanakijiji katika umilikaji na udhibiti wa ardhi na rasilimali asili yao. Hata hivyo, kama utafiti mwingi unavyodhihirisha, hali halisi ni kinyume. Ukweli ni kwamba serikali za kijiji huchukuliwa kama watekelezaji wa maagizo na maazimio kutoka juu (Halmashauri ya Wilaya na Serikali Kuu) badala ya watawala wa maeneo yao.
- 5) Hapo awali msimamo wa wataalam na watawala ulikuwa kwamba:-
- (a) Hifadhi ni suala la kitaalam, kwa hivyo, ni wajibu wa wataalam kuwaelekeza wenyeji/wananchi na kudhibiti na kupanga matumizi ya rasilimali asili.
 - (b) Rasilimali asili ni hazina ya taifa na ya kimataifa kwa hivyo msimamizi mkuu ni serikali kuu bila kujali matakawa na maslahi ya wenyeji.
- 6) Msimamo huo ndio ukazaa utawala kutoka juu kwa upande moja, na wenyeji/wanakijiji kuwa watekelezaji wa maagizo, kwa upande mwingine..
- 7) Utafiti mwingi sasa umedhihirisha wazi kwamba msimamo huo ulikuwa potovu kwa sababu wenyeji ndio wenye uzoefu mkubwa katika kuhifadhi mazingira na mali asili yao; kwamba hakuna binadamu atakaye kuwa tayari kujinyima wakati yeye mwenyewe hakushirikishwa wala haoni faida ya kufanya mambo yanoyoamrisha kutoka juu.

8) Kutokana na hayo kumetokea mabadiliko, angalau ya kinadharia, katika sera zima ya hifadhi, udhibiti na upangaji wa matumuzi ya rasilimali asili.

9) Msimamo wa kimaendeleo unasisitiza yafuatayo:

(a) Wenyeji na wanakijiji lazima washirikishwe katika mfumo mzima wa hifadhi na matumuzi ya rasilimali asili na ushirikishwaji huo hakuna budi uwe wa dhati. Kwa hivyo, wanakijiji weyewe ndio ni waamuzi wakuu katika masuala yote yahasuyo rasilimali asili.

(b) Upangaji na matumuzi ya rasilimali asili utoe kipau mbele kwa matakwa na maslahi ya wanakijiji wenyewe na taifa badala ya kujali mno maslahi ya wawekezaji au matakwa ya wahisani.

10) Ingawa msimamo huo wa kisasa ni wa kimaendeleo, utafiti huo umedhihirisha kwamba utekelezaji wake bado una walakin. Hasa mambo yafuatayo yanaashiria kwamba kunahaja ya uchambuzi wa kina na uchambuzi huo hauna budi uwashirikishe wanakijiji wenyewe moja kwa moja.

Kati ya mambo mengine, haya yafuatayo ni dosari katika utekelezaji wa msimamo mpya:

(a) Katika sera na sheria mpya kuhusu mfumo wa umilikaji wa ardhi, dola huendelea kumiliki ardhi yote ya Tanzania na wawekezaji hupewa kipaumbele katika upangiliaji wa matumizi ya ardhi. Wazalishaji wadogo vijijini - jamii za wakulima na

wafugaji - bado hukosa uhakika wa kutosha katika mfumo wa umilikaji ardhi.

- (b) Katika sera mpya ya misitu, wanyamapori na utalii, mwelekeo wa vyombo vya dola kuwa waratibu wakuu na waamuzi wa mwisho juu ya suala la rasilimali asili bado hupewa kipaumbele. Kwa hivyo, ushirikishwaji wa wanakijiji ni hafifu au wa kinadharia tu.
- (c) Wanakijiji huendelea kuwa na wasi wasi kwamba lugha ya hifadhi kutoka juu ni ile ile - yaani ni kisingizio cha kupora ardhi yao ama na idara za serikali au idara za serikali kwa manufaa ya wawekezaji hususun makampuni ya uwindaji au wachuuzi wa mazao ya misitu.
- (d) Wanakijiji bado hawaridhiki na hawaoni jinsi gani wao na jamii zao hufaidika na rasilimali asili yao.
- (e) Msukumo mkubwa wa mtazamo mpya hutoka kwa wahisani na wataalam wao ambao, hata hivyo, hukosa mwelekeo wa kitaifa na dira sahihi ya maendeleo. Kwa hivyo, suala muhimu ya umilikaji na usimamizi wa rasilimali asili hugeuzwa kuwa miradi ya wahisani na wanakijiji huendelea kuwa watekelezaji wa "ushauri" wa wataalam wahisani. (Mradi wa hifadhi ya msitu wa Mgori katika mkoa wa Singida ni mfano mzuri wa mwelekeo huo.)

Mapendekezo

Mapenkekezo ya mtafiti katika utafiti huo ambayo washiriki wanaombwa kujadili kwa undani na kuyakosoa ni yafuatayo:

1. Msimamo na mwelekeo wa mfumo wa umilikaji ardhi pamoja na rasilimali asili ubadilike kutoka ule wa uhodhi wa umilikaji na dola; badala yake wanakijiji kupitia chombo chao, hususun Mkutano Mkuu, ndio wawe wamiliki wa ardhi na rasilimali aisli. Watawala wawe washauri na wasiwe na uwezo wa kufanya maamuzi ya mwisho bila ridha ya wanakijiji.

2. Hifadhi na matumizi ya rasilimali asili sio mradi bali ni maisha yenyewe na suala la maendeleo ya wanakijiji katika jithada zao za kuinua masiha yao. Kwa hivyo, suala hili liwe sehemu ya mfumo wa utawala wa kijiji badala ya kuwekewa vyombo maalum vya muda na wataalam wahisani.

Wataalam wahisani ni wapita njia na miradi yao pia huufa mara baada ya wao kuondoka.

3. Kwa mantiki hii basi, suala la rasilimali asili na utawala bora wa kidemokrasia yanaambatana, sawa na pete ilivyo kwa kidole.

4. Udhibiti na usimamizi wa rasilimali asili uwe chini ya serikali ya kijiji ambayo ijibike kwa wanakijiji katika Mkutano Mkuu.

5. Mkutano Mkuu wa kijiji ndio wenye mamlaka ya mwisho kijijini na upewe uwezo wa kisheria kupitisha sheria ndogo ndogo za kuratibu matumizi ya rasilimali asili.
6. Katika miradi yote ya matumizi ya rasilimali asili (kwa mfano, uwindaji wa kibisahara, utalii n.k.) sheria itamke wazi hisa ya kijiji badala ya vyombo vya serikali kuu au serikali za mitaa kuamua mgawanyo wa mapato.
7. Sheria mama zitamke wazi uwezo wa kijiji kutoza na kukusanya kodi, ushuru n.k. ambao hutokana na matumizi ya rasilimali asili ili kijiji kiwe na uwezo wa kifedha kuboresha huduma kijijini. Kwa kifupi, vyanzo vya mapato ya kijiji viwe vinatajwa wazi na sheria na visiingiliwe na Halmashauri ya Wilaya au na idara zingine za serikali kuu.

Hitimisho

Uchmabuzi wa utafiti huo unadhihirisha kwamba suala la rasilimali asili ni sio wa kitaalam tu bali ni sehemu ya mfumo wa utawala na inaendana na sera na sheria ya kuboresha utawala wa kidemokrasia, uwazi na ujibikaji vijijini. Maana yake ni kwamba suala la udhibiti na matumizi bora ya rasilimali asili haliwezi kutatuliwa bila ya kuhusishwa moja kwa moja na suala la mabadiliko katika mfumo wa utawala bora vijijini. Isitoshe, nchi yetu haina njia nyingine ya kuondoa umaskini na kuleta maendeleo ya watu, bila kuweka vyombo vya ushirikishwaji wa wanakijiji katika utawala wao.

Kwa kifupi, basi, wanakijiji wajitawale badala ya kutawaliwa; wawe waamuzi badala ya watekelezaji tu; wawe wanufaishwa wa maendeleo

badala ya kuwanufaisha wengine na wawe na uwezo unaotambulika wazi wa kudhibiti, kusimamia na kuwajibisha warasimu na viongozi wao.
